

Novemba 2016



Wapendwa Marafiki,

Zaburi 100 inasoma:

“Zaburi ya shukrani. Mfanyieni Bwana shangwe dunia yote! Mtumikieni Bwana kwa furaha! Njooni mbele zake kwa kuimba! Jueni kwamba Bwana ndiye Mungu! Ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake! Tu watu wake, na kondoo wa malisho yake. Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru; Nyuani mwake kwa kusifu! Mshukuruni, lihimidini Jina lake! Kwa kuwa Bwana ndiye mwema; Rehema zake ni za milele, Na uaminifu wake vizazi na vizazi.”

Mwezi huu tunatenga muda kushukuru na kumsifu Mungu kwa yale yote anayofanya na aliyotenda kwenye maisha ya wanawake ulimwenguni kote na kwa vizazi vyote. Ni furaha iliyoje kuwa sehemu ya maombi haya na kumtukuza Mungu kwa yote aliyotenda kwa miaka 19 ya uwepo Project Hannah.

Leo, jiunge na wengine na uipaze sauti yako kumsifu Mungu. Mtumikie Mungu leo kwa moyo wenye furaha, na uingie kwenye uwepo wa Mungu ukiwa na wimbo kinywani mwako. Upendo wake kwako ni wa milele. Uweza wake ndani yako unazidi uwezo wowote ule ulimwenguni, na ukweli wake utadumu milele.

Yesu alikuja hapa duniani kuishi maisha yaliyodhihirisha upendo wa Mungu kwa ajili yetu. Yesu alitufia ili tuwe na uzima wa milele pamoja na Mungu milele yote. Tunaweza kuimba leo! Tunaweza kusifu leo! Tunaweza kuwa na matumaini leo!

Ninazo shukrani kwa ajili ya kila mmoja wenu mnapoitenga kila siku ya mwezi huu kwa ajili ya kusifu na kushukuru. Wewe ni wa muhimu sana kwenye huduma hii, na inafanya moyo wangu uimbe kwa furaha ukijua kuwa mnaziinua sauti zenu kwa kusifu na kushukuru kwa ajili ya wanawake ulimwenguni.

“O njooni tumwimbie Bwana, Tumfanyie shangwe mwamba wa wokovu wetu. Tuje mbele zake kwa shukrani, Tumfanyie shangwe kwa Zaburi. Kwa kuwa Bwana ni Mungu mkuu, Na Mfalme mkuu juu ya miungu yote. Mkononi mwake zipo bonde za dunia, Hata vilele vya milima ni vyake. Bahari ni yake, ndiye aliyeifanya, Na mikono yake iliumba nchi kavu. Njoni tuabudu, tusujudu, Tupige magoti mbele za Bwana aliyetuumba” (Zaburi 95:1–6).

Katika yeze mioyo yetu inashangilia,

Peggy Banks
Mkurugenzi wa Huduma Kimataifa
Project Hannah

Mtukuze Mungu kwa kile anachofanya kupitia waombaji waaminifu wanaoomba pamoja na timu ya maombi ya Project Hannah ya ulimwengu!

Vietnamu:

"Hatujawahi kusikia vipindi nya TWR moja kwa moja kwa njia ya redio; hata hivyo, tumepokea vipindi nya *Wanawake wa Matumaini* na kalenda za maombi zilizochapishwa kila wakati kwa miaka mitatu mfululizo sasa. Dada zangu hapa wanavipenda sana vipindi hivi, na sisi sote tunawaombea wahudumu wa *Wanawake wa matumaini* kila wakati tunapokutana. Tumeona wanawake wengi wana mabadiliko mazuri ya uvaaji, kuzungumza na watu kwa nidhamu, usafi wa kinywa na namna ya kuwatunza watoto. Kitu cha kipekee ni kwamba kila mmoja anasimama katika umoja kushiriki shida za kila familia kama kuwasaidia wagonjwa. Sisi wote tumeacha tabia mbaya tulizokuwa nazo kama kufukiza ubani kwenye makaburi ya ndugu zetu waliokufa, kutoa kafara, kuabudu mizimu na kufanya ibada za kitamaduni zilizotugharimu hela nyingi sana. Wanawake hapa hawajaacha tu kunywa pombe bali wamewatia moyo waume za kuacha kunywa pombe na kucheza kamari. Watoto wao pia wamekuwa na tabia njema na kundi letu sasa limeungana vizuri sana na kuwa imara."

"Mguu wangu wa bandia umeshatengenezwa, na ninafuraha sana. Asanteni sana kwa msaada wenu. Mke wake anajitolea kufuatilia na ni muwakilishi wa wanawake wa mkoa wetu pamoja 'Mama T,' muwakilishi wa mkoa mwingine. Huwa wanapokea kalenda za maombi za kila mwezi mara kwa mara na kuzisambaza. Kila mwezi, mke wake husambaza kalenda 20 za maombi na Mama T husambaza kalenda 50 kwa wanawake wa mkoani kwake ili waweze kuomba. Tunamshukuru sana Mungu."

Myanmar:

"Waombaji wa kikundi chetu cha Project Hannah wana fursa ya kushiriki kwenye mashindano ya kukariri mistari ya maandiko. Pamoja na kuomba kila siku kwa kutumia kalenda ya maombi ya kila mwezi, tunayo fursa ya kukusanyika kama kikundi kuomba siku za jumapili kanisani baada ya ibada ya asubuhi."

"Mungu awabariki wote! Ninawashukuru watu wa TWR Myanmar S'gaw Karen Project Hannah ambao huniletea kalenda za maombi za kila mwezi kwa wakati. Kila siku naombea mahitaji yake. Nimejifunza namna ya kuomba pia. Ninaomba kwamba watu wengi zaidi wajunge na vikundi nya maombi nya Project Hannah."

"Waombaji wenzetu wa vikundi nya maombi nya Project Hannah wanawaombea wanawake na wasichana ulimwenguni wanaoteseka kwa mambo magumu, shida na umaskini. Ninawahurumia wanawake na wasichana wanaoteseka ninapopata taarifa zao. Sina cha kufanya ili kuwasaidia zaidi ya kuwaombea. Waombaji wetu wana hamu kubwa sana ya kuomba. Kulingana na mpango wa Mungu, Timu ya TWR Myanmar ya Project Hannah ilitutia moyo kukusanyika pamoja na kuomba kama kundi moja. Kutokana na sababu hii, tunamtukuza Mungu na kuwashukuru sana watu wa TWR Myanmar wa Project Hannah. Kikundi chetu cha maombi cha Project Hannah hufanya mashindano ya kukariri mistari ya Biblia mara moja kila mwezi."